

**HOTUBA YA MGENI RASMI MKUU WA WILAYA YA GEITA  
MHESHIMIWA HERMAN KAPUFI KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU  
YA MTOTO WA AFRIKA HALMASHAURI YA MJI GEITA, KATA YA  
NYANGUKU TAREHE 16/06/2018**

- Mh. Mwenyekiti wa Halmashauri,
- Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji,
- Waheshimiwa Madiwani,
- Wakuu wa Idara,
- Viongozi wa Madhehebu ya Dini,
- Wakuu wa Mashirika /Makampuni na Taasisi za Serikali,
- Waheshimiwa watoto,
- Wageni waalikwa,
- Mabibi na Mabwana.

Ndugu wananchi, Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia nafasi hii ya kujumuika pamoja kwa lengo la kuadhimisha siku ya mtoto wa Afrika. Napenda kushukuru kwa dhati kabisa wananchi wa Nyanguku kwa kukubali kuwa wenyeji wa maadhimisho haya. Aidha ninawashukuru wadau wote walioacha shughuli zao na kuamua kujumuika nasi katika maadhimisho haya, Karibuni sana tujumuike pamoja.

Ndugu wananchi, siku hii ya Mtoto wa Afrika huadhimishwa kote Barani Afrika tarehe 16 Juni ya kila mwaka. Hii ni kwa makusudi ya kutekeleza azimio la Umoja wa Nchi huru za Afrika katika kuwakumbuka watoto wa Kitongoji cha Soweto – Afrika ya Kusini waliouwawa kinyama tarehe 16 Juni, 1976 wakati wakidai haki yao ya kutokubaguliwa na haki nyingine za msingi

zikiwemo kupewa Elimu, huduma za Afya, kusikilizwa, kupendwa na kulindwa.

Ndugu wananchi, kauli mbiu ya mwaka huu 2018 inasema "**Kuelekea Uchumi wa Viwanda: Tusimwache mtoto nyuma**" kauli mbiu hii inatumkumbusha umuhimu wa ushirikishaji wa watoto katika ubunifu na kukua wakiwa wabunifu ili tuweze kuzalisha wataalam wengi ambao watasaidia kuendeleza nchi yetu kiuchumi, naamini nyote mmeona shughuli walizotengeneza vijana wetu, tutakaposhikamana nao na kuthamini juhudi zao watasaidia kuendelea mpango wa Serikali wa kuwa nchi ya viwanda.

Ndugu wananchi, nchi yetu inaendelea kupiga hatua kiuchumi kufikia uchumi wa kati, uwepo wa viwanda utasaidia kuongeza kasi ya maendeleo ya nchi yetu. Malezi na makuzi ya watoto ni muhimu katika maendeleo ya nchi. Watoto wanatakiwa kujengewa uwezo toka wakiwa wadogo katika dhana mbalimbali za uzalishaji mali ili tuweze kuzalisha wataalam wengi wenye tija kwa masilahi ya nchi yetu.

Ndugu wananchi, mtoto ana haki ya kulindwa, haki ya kulindwa inahusu kuzuia vitendo viovu wanavyofanyiwa watoto. Ulinzi huo unahitajika katika hatua za ukuaji wake kabla na baada ya kuzaliwa. Aidha, mtoto anahitaji ulinzi dhidi ya unyanyasaji, vitendo vya kikatili, ukeketaji watoto wa kike, mimba na ndoa za utotoni, matumizi ya madawa ya kulevya na vitendo vya ubakaji.

Ndugu wananchi, kumefanyika harakati nyingi za kukomesha vitendo vya kikatili dhidi ya watoto lakini bado vinaendelea na kutishia amani, utulivu na uhuru kutokana na kulindana katika familia. Hivyo Serikali itaendelea kuchukua hatua kali kwa wote watakaohusika, napenda kuwasisitiza wazazi

na walezi kwamba mnatakiwa kuwalinda na kuwatunza watoto wenu kwa kuwahakikishia usalama wao.

Ndugu wananchi, watoto wana haki ya kushirikishwa katika mambo yanayohusu maendeleo yao. Ni wazi kwamba wazazi, walezi na Jamii hawatoi fursa ya kutosha kwa watoto ili waweze kutoa mawazo na michango yao katika maamuzi mbalimbali yanayohusu maendeleo yao na familia. Hali hii inatokana na dhana kwamba watoto hawana uelewa na uwezo wa kuchangia katika maamuzi mbalimbali kuanzia ngazi ya familia na jamii kwa ujumla, jambo ambalo limewanyima watoto haki yao ya kushiriki.

Ndugu wananchi, mmomonyoko wa maadili katika jamii, unachangiwa pamoja na mambo mengine mifarakano katika familia, kuvunjika kwa ndoa, ugumu wa maisha na utandawazi. Mmomonyoko huu wa maadili husababisha kuwepo na ongezeko kubwa la watoto wanaozaliwa nje ya ndoa, tendo ambalo linasabababisha watoto kutotambulika kisheria na hivyo kunyimwa haki zao. Vilevile husababisha watoto kuiga tabia zisizofaa, kujiingiza katika vitendo vibaya kama vile ukahaba, ubakaji, mauaji, wizi, utumiaji wa madawa ya kulevyia, pombe na sigara. Aidha, ni muhimu kuhakikisha kwamba watoto wanajengewa mazingira mazuri ya kiafya, kielimu, kimaadili, kisaikolojia na kiroho ambayo yatawezesha kuwa na ustawi na maisha bora.

Ndugu wananchi, mwisho napenda kuwakumbusha kuwa jukumu la kuwalinda watoto ni la kila mmoja wetu. Kwa hiyo natoa wito kwa wadau wote wa Maendeleo ya mtoto kuunga mkono jitihada zilizoanzishwa na Serikali na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali katika kuwalinda watoto na kutoa fursa kwa wote bila ubaguzi.

Ninawakumbusha kuwa vitendo vyote vya ukatili, unyanyasaji, udhalilishaji na dhuluma ya namna yoyote dhidi ya watoto ndani na nje ya familia haviwezi kamwe kukubalika katika jamii yoyote ya Tanzania. Badala yake tujikite katika kuwafundisha watoto wetu kazi ambazo zitakua na manufaa kwa maisha yao ya baadae na Taifa kwa ujumla kama tunavyokumbushwa kuwa **'kuelekea uchumi wa Viwanda: Tusimwache nyuma mtoto.**

**MUNGU IBARIKI AFRIKA**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**MUNGU IBARIKI GEITA**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**